

Toleo la. 17

Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKLEZA | APEWE TENA 5 | 18 SEPTEMBER, 2020



KICOMA WAGOMEA UNAFIKI, WASEPA NA JPM



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**

TAHARIRI

LA MANUFAA YA NDEGE LIMEISHA HILOOOOOO!!!

Bango alilobeba mwananchi mmoja wa Kigoma leo kwenye mkutano wa Mgombea Urais wa CCM, Ndugu John Pombe Magufuli limemaliza ubishi kuhusu manufaa ya ndege zilizonunuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Katika bango hilo mwananchi huyo alionesha juu jinsi Mwanasiasa Zitto Kabwe alivyokuwa akiponda ununuzi wa ndege hizo na hata wakati fulani kudai ni mbovu lakini juzi na mara kadhaa akanaswa akiwa amepanda ndege aina ya Bombardier na akishuka katika Uwanja wa Kigoma akitokea Dar.

Si Zitto tu, katika kile kinachoonekana kuendeleza hoja muflisi, wanasiasa wengi wengine waliokuwa nao wakifuata mkumbo na kuponda ndege zetu na hata kujaribu kuzihujumu zishikwe na wadeni wetu akiwemo Tundu Lissu katika kampeni hizi wamejikuta ndege ndio zinawakomboa kwa kuzitumia kuwahi katika mikutano yao ya mbalimbali ya kampeni.

Mbali na kuonekana akiwa anashuka kwenye ndege ya ATC, clipu moja iliyosambaa majuzi mitandaoni ilieleza jinsi mmoja wa abiria aliyekuwa ndani ya ndege hiyo pamoja na Zitto alimvyomshuhudia mwanasiasa huyo akihaha huku na kule akiwa ndani ya ndege; mara aombe kwenda chooni, mara aombe kuongezewa juisi, korosho na maji, ilimradi tu akifaidi matunda ya kazi na ubunifu wa Rais Magufuli ambao kwa nje unapinga.

Tunaamini, wanasiasa wana michezo yao ya kisiasa, lakini moyoni wanajua kuwa Serikali imetekeleza jambo kubwa kwa kununua ndege hizi nane zilizoko nchini na tatu ambazo zitafika wakati wowote kuanzia mwaka huu.

Hata hivyo, pamoja na siasa, tunawakumbusha wanasiasa kuwa yako mambo ya msingi kitaifa hawapaswi kutafanyia mzaha au kuyabeza, moja wapo ni hili la ndege. Ndege ni ajira, ni biashara, ni uchumi na zaidi ni mapato kwa Serikali.

Tunaamini kwa yaliyotokea Kigoma leo kwa wananchi kupaza sauti kulinga uzandiki wa Zitto na wenzake, hili la ndege sasa ni sawa na kusema: "Imeisha Hiyooooooooooooooooo."





MAGUFULI KUIFUNGUA KIGOMA KIBIASHARA

- Kujenga Meli Mbili Kubwa, Uwanja wa Ndege Kupanuliwa
- Kuigeuza Kigoma Kuwa Kitovu cha Biashara

Na Mwandishi Wetu - **KIGOMA**

Mgombea Urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ameahidi kuimarisha miundombinu ya usafishaji na uchukuzi katika mkoa wa Kigoma ili kuufanya mji huo kuwa kitovu cha biashara.

Rais Magufuli amsema hayo leo alipokua akinadi Sera za CCM na kuomba kura kwa wananchi wa Kigoma waliofurika katika Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma ambapo ameeleza kwamba endapo atachaguliwa tena atajenga meli kubwa mbili, atapanua Uwanja wa Ndege wa Kigoma, atajenga barabara na reli sambamba na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za jamii.

“Hapa Kigoma tumepanga si kununua meli mpya tu, bali kukarabati meli ya MV Liemba iwe mpya kabisa kwa gharama ya shilingi bilioni 10. Pia tutakarabati meli ya MV Sangara kwa gharama ya shilingi bilioni sita, tutajenga majengo ya kisasa ya Ofisi za Bandari Kigoma, lengo ni kuifungua Kigoma kuwa eneo la kibiashara na kukuza utalii kupitia meli hizi na ndege zetu,” alieleza Mhe. Magufuli.

Kuhusu usafiri wa anga, Rais Dkt. Magufuli amesema kuwa uwanja wa ndege wa Kigoma utapanuliwa na kwamba jengo la kisasa lenye ghorofa tatu litajengwa, sambamba na kuwekwa taa na miundombinu ya kisasa ili kuwezesha ndege kubwa zaidi kutua na hivyo kuchochea utalii kukua kwani mkoa huo una vivutio vingi.

Amesema Kigoma imenufaika na mradi wa uendelezaji miji nane ya kimkakati ambapo barabara zenye urefu wa kilomita 15.13 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kuwekwa taa sambamba na kujenga dambo la kisasa, huku miradi yote ikigharimu shilingi bilioni 31.19.

Mbali na hayo, Serikali ya Rais Dkt. Magufuli imetumia shilingi bilioni 18.27 ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya, shilingi bilioni 13 katika miradi 25 inayoendelea katika vijiji mbalimbali, huku sekta ya elimu ikinufaika kupitia ujenzi wa madarasa 323, nyumba za walimu 53, mabweni 38, maabara 19, makataba mbili, kukarabatiwa kwa shule Kongwe mbili na pia walimu 1,728.



VIONGOZI WA DINI WAPONGEZA MAENDELEO YA VITU

Na Mwandishi Wetu - KIGOMA

Viongozi wa dini mkoani Kigoma wamepongeza maendeleo ya vitu yaliyoletwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika miaka mitano iliyopita ambayo yamesaidia kuinua maisha ya watanzania huku wakimuomba Mwenyezi Mungu ampe ushindi wa kishindo ili aendeleze kazi ya kujenga Tanzania.

Pongezi hizo zimetolewa leo na Sheikh wa Mkoa wa Kigoma, Sheikh Hassan Kiburwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Makanisa ya Kipentekoste, Askofu Charles Katale wakati wakisoma sala na dua kabla ya kuanza kwa mkutano wa kampeni za gombea Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Pombe Magufuli, uliofanyika kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika uliopo Kigoma mjini.

"Mwenyezi Mungu sote tunajua maendeleo ya kweli yanatokana na vitu kwanza kisha watu, hata wewe Mola wetu kabla ya kutuumba ulituwekea vitu mbalimbali ili utuendeleze kama wanadamu, na ndivyo mtumishi wako huyu (Rais Dkt. Magufuli)

mnyenyekevu anavyofanya," alieleza Sheikh Kiburwa katika sehemu ya dua aliyoimba.

Nae Askofu Katale alimuomba Mungu akisema: "Tunawaomba vipofu waone yale yaliyofanyika, viziwi wasikie kazi nzuri zilizofanyika katika nchi yetu, namuomba Rais wetu John Pombe Magufuli ulinzi katika kazi zake, ahsante Mungu, nawaomba wakazi wa Kigoma wote wampe Rais Magufuli kura zote za ndio".

Tangu Rais Magufuli aingie madarakani miaka mitano iliyopita, ametekeleza miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa barabara ili kurahisisha usafiri na usafirishaji, ujenzi na ukarabati wa shule pamoja na madawati ili wanafunzi wawe na maendeleo kwa kupata elimu katika mazingira bora, ujenzi wa hospitali, ununuzi wa dawa na vifaa tiba ili kujenga Taifa la watu wenye siha njema watakaofanya kazi ya kujiletea maendeleo na pia amenunua ndege ambazo kwa kiasi kikubwa zimerahisisha usafiri wa watu kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa muda mfupi.



TULIDHAMIRIA KULIFUFUA ZAO LA CHIKICHI - MAGUFULI

Na Mwandishi Mahususi - KIGOMA

Mgombea Urais wa kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Pombe Magufuli amewaeleza wananchi wa Kigoma kuwa Serikali yake ilipoingia tu madarakani mwaka 2015, iliweka mikakati ya kulifufua zao la Chikichi kwa lengo la kukuza zao hilo la biashara pamoja na kuinua maisha ya wananchi wa mkoa huo.

Rais Magufuli amebainisha hay oleo alipokua akinadi Sera za Chama chake pamoja na kuomba kura kwa wananchi katika mkutano wa kampeni uliofanyika kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma.

"Tulipoingia madarakani tuliamua kufufa zao la Michikichi hapa Kigoma maana ndio zao la biashara hapa na kwa sababu nataka Kigoma ipande juu na watu wa Kigoma watajirike," alieleza Rais Magufuli.

Pamoja na Serikali yake kulifufua zao hilo, Rais Magufuli amewaeleza wananchi wa Kigoma kuna amesikia kuna baadhi ya watu wanasema wao ndio waliolifufua zao hili na hivyo kuwataka wananchi wa Kigoma kutowasikiliza kwani haomni matapeli wa kisiasa.

"Nawaomba ndugu zangu mjiepushe na matapeli wa siasa, kwenye siasa matapeli wapo ndio maana nawaeleza ukweli asije mtu akawadanga miradi hii kaileta yeye," alisisitiza.

Katika kuhakikisha zao la Chikichi linaimarika na kunufaisha wananchi, Serikali ya Rais Magufuli imeanzisha Kituo cha utafiti wa zao katika eneo la Kihinga mkoa wa Kigoma ambapo mpaka sasa zaidi zaidi ya miche ya kisasa milioni 1, 800,000 imezalishwa.



KIGOMA WAFUNIKA MKUTANO WA MAGUFULI

Na Mwandishi Mahususi - KIGOMA

Mamia ya wakazi wa Mkoa wa Kigoma wamehudhuria mkutano wa hadhara wa kampeni za Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Magufuli huku Uwanja ukifurika na umati mkubwa ukijipanga pembezoni mwa barabara za mji huo kwa kumpokea mgombea huyo.

Mkutano huo umefanyika leo katika Uwanja wa Lake Tanganyika uliopo Kigoma Mjini na kuhudhuriwa pia kuhudhuriwa na wagombea Ubunge na Udiwani, viongozi wa dini, machifu, wazee, vijana, wasanii, madereva bodaboda, wananchi kutoka makundi mbalimbali ambapo wengi wao walivaa nguo za CCM na wengine kubeba mabango ya kumpongeza Rais Magufuli.

Baadhi ya wananchi walikua na mabango yenye jumbe mbalimbali likiwamo liloandikwa "Kazi lendelee" pamoja na linalomuonesha mgombea Ubunge Jimbo la Kigoma Mjini, Zitto Kabwe akishuka kwenye moja ya ndege.

Ifahamike kwamba Zitto Kabwe ni mgombea Ubunge wa Jimbo la Kigoma Mjini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo ambae amekuwa akipinga maendeleo yaliyoletwa na Serikali ya Awamu ya Tano, ikiwemo ununuzi wa ndege ambazo zimekuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa Kigoma katika suala la usafiri.

Akizungumzia kuhusu maendeleo yaliyoletwa na Serikali ya Awamu ya Tano, mmoja wa madereva bodaboda waliohudhuria mkutano huo, Bw. Ezaeli Mtengu amesema kuwa Tanzania imebahatika kuwa na Rais anayependa maendeleohivyo ni muhimu watanzania wakalionga hilo na kumuunga mkono.

"Rais wetu amefanya kazi kubwa sana. Hapa Kigoma kuna miradi mingi inaendelea ikiwemo lami ambayo inatufanya hata sisi wa bodaboda tupite kwa raha. Tunashangaa kuona mtu anasema eti kwa nini Serikali imenunua ndege wakatisasa hivi ndege za ATCL tunaona zikitua hapa na hata juzi tumemuona Zitto akishuka kutoka katika ndege yetu anayoipinga,"

Anaeleza kuwa wao kama madereva wa bodaboda Rais Magufuli amewasaidia sana kwani zamani walikuwa wanakikimbizwa na kupigwa askari lakini sasa hivi askari hao wamekua kama ndugu zao kwa jinsi wanavyowapa ushirikiano.



BILIONI 1.8 ZAJENGA HOSPITALI YA KISASA NYASA

• Inatoa huduma za Kibingwa kwa Wakazi wa Nyasa

Na Mwandishi Wetu - RUVUMA

Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 1.8 kujenga hospitali ya Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma, ambayo pia inatoa huduma za kibingwa kwa wakazi wa wilaya hiyo ambao hawajawahi kupata huduma hizo kwa zaidi ya miaka 59 tangu Tanzania ipate uhuru.

Akiuhutubia mkutano wa kampeni uliofan- yika katika Kijiji cha Liuli Jimbo la Nyasa Mkoani Ruvuma, Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema lengo la kujenga hospitali hiyo ni kuhakiki- sha wananchi wa Wilaya ya Nyasa wana- pata huduma bora za afya zikiwemo zile za kibingwa.

Ameeleza kuwa bado Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kuboresha sekta ya afya na kuwaomba wakazi hao kumcha- gua Dkt. John Pombe Magufuli ili kukamil- isha lengo hilo kuwasogezea karibu wana- nchi huduma za afya.

Pamoja na kukamilika kwa baadhi ya

miradi wilayani humo, Mhe. Samia ame bainisha kuwa Serikali pia inaendelea kujenga zahanati kila kijiji kwenye vijiji 84 vya wilaya ya Nyasa na vituo vya afya vya Mkiri na Kihagara pamoja na kuimarisha wodi ya wazazi ya kituo cha afya Mbamba Bay kwa lengo lilelile la kuwapatia watan- zania huduma bora za afya.

"Ndugu zangu wa Liuli, ni Serikali ya CCM pekee ndiyo inayojali maisha ya watanza- nia, ni Serikali ya CCM pekee ndiyo inayoweza kuyafanya haya, sio mtu mwingine, mchagueni Dkt John Pombe Magufuli aongeze maendeleo hapa Nyasa na Tanzania kwa ujumla, chagueni Wabunge na Madiwani wa CCM pia" alisisitiza Mhe. Samia.

Wakazi hao ambao walikuwa wakipata huduma hizo kwa taabu huku wakilazimi- ka kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita 100 kufuata huduma katika hospi- tali za Litembo, wilaya ya Mbinga na Songea Mjini, sasa wanafurahia huduma hizo zikiwa jirani na maeneo wanayoishi.



MELI YA MV MBEYA TAYARI KUANZA KAZI

Na Mwandishi Wetu - RUVUMA

Serikali imeanza kuifanyia majaribio Meli mpya ya abiria ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo, itakayofanya safari zake kwenye Ziwa Nyasa kuanzia Bandari ya Itungi iliyo-po wilaya ya Kyela mkoani Mbeya hadi Mbamba Bay wilayani Nyasa Mkoa wa Ruvuma.

Akihutubia wakazi wa Liuli na Mbamba Bay wilayani Nyasa Mkoani Ruvuma, Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muun-gano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali itafanya mazungumzo na nchi jirani ya Malawi ili kuangalia uwezekano wa meli hizo zifike nchini humo kusafirisha mizigo na abiria.

"Katika Ziwa Nyasa tumefanya ujenzi wa Meli mpya tatu ikiwepo moja ya abiria na mbili za mizigo. Meli za mizigo tayari zimeshaanza kazi na moja ya abiria tunai-fanyia majaribio ili iweze kufanya kazi hivi karibuni, tunatambua changamoto za usa-firishaji huku Nyasa na ndio maana tume

-kuja na mpango huu, mchagueni Dkt. John Pombe Magufuli ili aendelee maendeleo haya," alieleza Mhe. Samia.

Meli ya MV Mbeya II ni kati ya Meli tatu mpya zilizoundwa na Serikali ya Awamu ya Tano chiniya Dkt. John Pombe Magufuli katika Ziwa Nyasa kwa gharama ya shilingi bilioni 20.1, nyingine mbili ni Meli za mizigo zote zikiwa na uwezo wa kubeba tani 1,000 za mizigo ikiwepo Meli ya MV Njombe na MV Ruvuma.

Katika hatua nyingine, Mhe. Samia amesema Serikali imeanza ujenzi wa gati katika Kijiji cha Ndumbi kilichopo Kata ya Mbaha Wilayani Nyasa Mkoa wa Ruvuma kwa gharama ya shilingi Bilioni 12.180 ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 15.

Amesema lengo la Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wananufaika na Ziwa Nyasa kiuchumi kupitia sekta ya Usafirishaji wa majini na Uvuvi ambao umeimarishwa sana katika miaka miano iliyopita.



MAJALIWA: CHAGUENI KIONGOZI ATAKAYEDUMISHA AMANI

Na Mwandishi Wetu - **BUNDA**

Watanzania wameaswa kumchagua kiongozi atakayemuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kudumisha amani na umoja kwa maslahi ya waTanzania wote.

Akizungumza kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika kwenye Jimbo la Bunda mkoani Mara leo, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amesema mgombea anaeweza kudumisha mawili hayo anapatikana CCM pekee.

“Chama cha Mapinduzi kina hazina na utaratibu mzuri wa kuwaandaa viongozi wake, hivyo nawasihi wana-Bunda mumchague Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kipindi cha pili cha miaka mitano ili akamilishe kazi alizozianza na pia aendelee kulinda amani na umoja wetu”, alisisitiza Mhe. Majaliwa.

Amesema Tanzania ni nchi ya amani hivyo tuna jukumu la kuendelea kuifanya kuwa sehemu ya kimbilio la nchi jirani.

5 KALI ZA MAGUFULI MKOANI KIGOMA SEPTEMBER 18, 2020.

01

Miradi hii ya ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 15.13, uwekaji taa za barabarani, ujenzi wa Dampo la kisasa hapa Kigoma mjini vimetekelezwa chini ya programu ya uendelezaji miji 8 ya kimkakati, Jumla ya shilingi bilioni 31.19 zimetumika kutekeleza miradi hii.

02

Mradi wa maji kutoka ziwa Tanganyika umefikia asilimia 95 na unazalisha lita za ujazo milioni 18, ukikamilika utazalisha lita za ujazo milioni 40 wakati mahitaji ya mkoa wa Kigoma ni lita za ujazo 23. Miradi ya maji 25 inaendelea katika vijiji mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 13. Aidha, katika bajeti ya mwaka huu imetengwa shilingi bilioni 54.12 kwa ajili ya kushughulikia tatizo la maji katika mkoa huu.

03

Hapa Kigoma katika miaka mitano ijayo, tumepanga kununua meli mbili kubwa ambazo zitafanya kazi kwenye ziwa Tanganyika, tutakarabati meli ya MV Lyemba iwe mpya kwa shilingi bilioni 10 na tutakarabati vizuri zaidi meli ya MV Sangara kwa gharama ya shilingi bilioni 6. Mimi sitoi ahadi hewa, nataka Kigoma niifungue najua siku moja mtanikumbuka.

04

Katika ziwa Tanganyika tutajenga pia bandari ya Kalema, Kabwe, Kasanga ambazo zipo katika Mkoa wa Rukwa na Katavi. Pia tuna mpango wa kuupanua tena uwanja wa Kigoma kwa kuuongeza urefu, jengo la abiria la ghorofa na tutaweka taa kwenye uwanja huo ili ndege kubwa ziweze kutua, kuna mbuga za wanyama hapa hivyo usafiri wa ndege ndio utaleta watalii.

05

Nawaomba ndugu zangu mjiepushe na matapeli wa siasa, kwenye siasa matapeli wapo ndio maana nawaeleza ukweli asije mtu akawadanganya miradi hii kaileta yeye.



MAJALIWA AANIKA MAFANIKIO YA SERIKALI BUSEGA

- Asema Miradi ya Maji Busega Imetumia Shilingi Bilioni 3.7

Na Mwandishi Wetu - **SIMIYU**

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa amesema shilingi bilioni 3.7 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika wilaya ya Busega. Ametoa kauli hiyo leo kwa nyakati tofauti alipokuwa akizungumza na wakazi wa kata za Mkula na Lamadi, wilaya ya Busega, mkoani Simiyu alipokua njiani kuelekea wilayani Bunda, mkoani Mara.

Mhe. Majaliwa amesema fedha hizo zimetumika kujenga mradi wa maji bomba katika kijiji cha Lukungu ambao tayari umekamilika. Pia fedha hizo zilitumika kufanya ukarabati wa chanzo cha maji katika mradi wa maji wa Kalemela-Mkula ambao nao tayari umekamilika. Ameitaja miradi mingine kuwa ni mradi wa maji bomba Kiloleli unaohudumia vijiji vitatu vya Ihale, Ijitu na Yitwimila B ambao pia umekamilika.

Amesema fedha hizo zimetumika kufanya upanuzi wa mradi wa maji Lamadi (Kalago na Mwa-bayanda) ambao umefikia asilimia 50, upanuzi wa mradi wa maji Nyashimo ambao umefikia asilimia 10, ujenzi wa mradi wa maji Mkula sekondari ambao umefikia asilimia 60 na mradi wa maji Bushgwamhala ambao umefikia asilimia 100.

Kuhusu umeme, Mhe. Majaliwa amesema kati ya vijiji 59, vijiji 53 vimeshapelekewa huduma ya umeme na vijiji sita bado havina umeme na tayari vimeingizwa kwenye mpango wa kupelekewa umeme. Wakati huohuo, Mhe. Majaliwa amesema ili kuboresha miundombinu ya barabara katika wilaya hiyo mpya, shilingi bilioni 2.3 zimetolewa kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Amesema fedha zilizotolewa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara zilihusisha barabara za Mwamanyili - Busami; Masanza Sec. School - Sayaka Road; Nyamikoma - Busega na Lamadi Secondary School-Suti Moja. Barabara nyingine ni Masanja-Ashico Petrol Road Malili- Mwa-migongwa-Ng'wang'wenge, Nyang'haya-Kasoli na Ngong'ho-Ndono Petrol Station.

Mhe. Majaliwa ametumia fursa ya kuongea na wananchi kumuomba kura mgombea Urais kwa tiketi ya CCM, Dkt. John Pombe Magufuli, mgombea Ubunge wa jimbo la Busega, Bw. Simon Songe na wagombea Udiwani wa kata zote za wilaya ya Busega.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**